**Sikiliza Ujifunze - Mazingira na Hali ya Hewa**
**07 - Deforestation (Ukataji wa Misitu)**
**Text: Richard Lough**
**Redaktion und Idee: Johannes Beck**
**Translator: Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi maalum vya Sikiliza na Ujifunze ambavyo huangalia masuala ya mazingira.Leo hii tutasikiliza juu ya taathira mbaya kwa mazingira kutokana na ukataji wa misitu.

Katika miaka ya 1980 na 1990 Afrika ilipoteza misitu zaidi kuliko bara lobte lile duniani ikiwa ni matokeo ya kuongezeka kupindukla kwa mahitaji ya kuni za kupikia,ardhi ya malisho kwa wanyama na mbao.Misitu ya Afrika inaendelea kukatwa katika kiwango cha kutisha.

Leo hii, radionovela itasimulia juu ya kampuni za mbao zisizo halali au kwa maneno mengine zinazoendesha shughuli zake kinyume na sheria barani Afrika. Kadhalika tutapata ukweli huu na takwimu kutoka kwa mwandishi wa Radio Deutsche Welle aliyeko Kenya Richard Lough. (anatamkwa Lock).

**Music — 0:30**

**SFX: Television background noise - sauti ya TV ikisikika kwa mbali**

**Monica**: Moses televisheni yenu mpya na kifaa cha kuchezesha DVD ni vizuri! Mara ya mwisho nilipokuja hapa televisheni yenu ilikuwa ya zamani na kioo chake kilikuwa na ufa.

**Moses:** Ni kweli lakini sasa baba amepata kazi mpya na tumeukata sasa tumekuwa matajiri.

**Gladys:** (exclaims - anatamka kwa mshangao) He! Mmetajirika kwa haraka mno!

**Monica:** Enhh kwa haraka sana!

**Gladys:** (curious - akidadisi) Lakini mmetajirika kwa kufanya nini hasa?

**Moses:** Kampuni ya mbao hiyo iliyotuneemesha. Baba anafaya kazi na kampuni ya kukata miti ilioko kama kilomita 30 hivi kutoka hapa katika msitu huko Malabar.Baba anasema mbao hizo huuziwa China na Ulaya.

**Monica:** **(SFX: slams her cup on the table - anagonga kikombe chake mezani)** Je unajua uharibifu unaofanywa na kampuni hizo za mbao kwa mazingira yetu?

**Moses:** (defensive - akitetea) Nini? Hiyo ni misitu tu! Baba anasema China ina uchumi unaokuwa kwa haraka kabisa duniani. Wanahitaji mbao kwa ajili ya vitu vya ujenzi na kutengeneza fanicha. Ni fedha inayopatikana kwa urahisi kwa jamii yetu ya kimaskini!

**Monica:** Fedha rahisi (anaguna) hmmmm! Lakini misitu hiyo katu haiwezi tena kurudia hali yake ya kawaida!

**SFX: Television switched off - TV inazimwa**

**Monica:** Twendeni

**Moses:** Wapi?

**Monica:** Kwenye kiwanda chenyewe. Tutakwenda pamoja na kaka yangu Soloman, yeye anafanya kazi na mradi mmoja wa jumuiya ya wenyeji kuokoa misitu.

**SFX: Door Closes X-fade into sound of travelling vehicle .... Mlango unafungwa, changanya na sauti ya gari linaloondoka.**

**Moses:** Unaona, hapo kabla kulikuwa hakuna hata barabara ya kuelekea Malabar ilibidi tutembee kwa miguu kwenda huko.

**Soloman:** Na unafikiri nani amelipia ujenzi wa barabara hiyo? Bila ya shaka ni kampuni za mbao ili kwamba ziweze kuikata misitu yetu na kuiacha ardhi iwe tupu kabisa na kuzichukua mbao na kuzisafirisha nje ya nchi haraka iwezekanavyo.

**Moses:** Lakini angalau tunaweza kwenda hapa na pale kwa urahisi zaidi.

**Soloman:** Labda, lakini kwa kujenga barabara mpya kampuni za mbao zinazidisha uharibifu wa misitu yetu.

**Gladys:** Kwa vipi?

**Soloman:** Kwa sababu ghafla watu wanakuwa wanaweza kuyafikia maeneo mapya. Idadi ya watu wetu inaongezeka na watu wanahitaji nafasi zaidi hususan wafugaji wa ng’ombe ambao wanatafuta maeneo mapya ya kuchunga mifugo yao.

**Monica:** Angalia unaweza kuona pembezoni mwa barabara tayari wanatia moto mashamba madogo.

**Soloman:** Dereva tafadhali simamisha gari hapa.

**SFX: Vehicle slows to halt, Door opens X-fade into loud machinery Gari linapunguza mwendo changanya na sauti kubwa ya mlio wa mashine**

**Gladys:** (Gasps ....Duwaa) Angalia kwenye uzio ule. Ardhi ni tupu!

**SFX: Walking across grass - Wakitembea kwenye nyasi**

**Soloman:** Mbao wanazozitafuta ni za Mkangazi. Ni mbao ngumu ambazo hupatikana Afrika na Amerika ya Kusini. Ni mojawapo ya miti yenye bei ya juu kabisa katika soko la mbao duniani. Fanicha zinazotengenezwa kwa mti wa Mkangazi zinauzwa kwa bei ndogo huko Ulaya na Marekani lakini hivi sasa mahitaji yake yanaongezeka nchini China.

**SFX: chainsaw and falling tree - sauti ya msumeno na mti kuanguka**

**Soloman:** Umri wa miti hiyo ingelikuwa ni mamia ya miaka. Kampuni hizi huwa zinatakiwa kuchagua ni miti gani ya kuikata na kuibakisha mingine. Lakini badala yake huwa wanaendesha shughuli zao katika kiwango cha juu sana kwamba huwa tu wanakata kila kitu na kuiacha ardhi kuwa tupu.

**Gladys:** Je huwa hawajali kwamba wanaharibu makaazi ya asili ya wanyama wengi ukiachilia mbali mazingira yetu ya kuishi?

**Soloman:** Hapana. Sina hakika kama wanajali kwani huwa wametawaliwa na tamaa ya faida. Kuna taratibu zinazoelekeza kampuni hizo jinsi ya kukata miti.

**Moses:** Kwa hiyo kwa nini hawazifuati?

**Soloman:** Kwa sababu mara nyingi huwa wanaweza kuwahonga maafisa wa serikall za mitaa ili wafumbie macho utendaji wao. Hebu njoo nataka kukuonyesha uharibifu unaosababishwa na ukataji wa miti.

**SFX: Walking across grass ...Wakitembea kwenye nyasi**

**Monica:** Nimesikia pia Soloman kwamba ukataji miti huwa unaharibu pia kiwango cha ubora wa ardhi.

**Soloman:** Hilo ni kweli. Wakati unapoondoa mimea kwenye eneo udongo unakuwa rahisi kumomonyoka.

**Moses:** Hiyo inamaanisha nini?

**Soloman:** Unajua miti na mimea husaidia kushikamanisha udongo pamoja wakati mvua inaponyesha. Wakati unapong'oa mimea maji ya mvua husomba sehemu ya juu ya ardhi. Katika baadhi ya sehemu ya bara la Afrika maeneo yote ya nchi ardhi yake hayana rutuba.

**Monica:** Na ardhi iliobakia kiwango cha ubora wake kinakuwa kibaya au sio?

**Soloman:** Sawa kabisa inakuwa haina rutuba kabisa kwa sababu inakuwa haina virutubishi.

**Gladys:** Wiki iliyopita nilikuwa mtoni, ule mto ambao unatiririka kufuata bonde kule chini. Maji yake yalikuwa mazito rangi nyekundu ....kidogo kama rangi ya kutu hivi. Tunaweza kwenda tena kwenye mto ute?

**SFX: Hum of agreement - sauti ya makubatiano**

**SFX: Walking through mud … wakitembea kwenye matope**

**Soloman:** Pale ndipo wafanyabiashara wa mbao walipokuwa wakikata miti mwaka jana.

**Gladys:** Na ardhi iko tupu kabisa na angalia korongo imekwenda chini mno

**Moses:** Wakati kwa upande wa pili wa bonde miteremko bado ina misitu minene. Mnadhani baba yangu anapaswa kulaumiwa kwa yote hayo?

**Soloman:** Hapana, sio baba yako. Mara nyingi kampuni hizi kubwa huwa zinataka kujinufaisha na nchi zinazoendelea na watu wake. Wao haja yao iko katika mbao tu. Baba yako huenda akawa hajui juu ya athari zake za kimazingira. Lakini viongozi wakuu wa kampuni hizo wanajua.

**X-fade into SFX river water … changanya na sauti ya maji ya mto**

**Moses:** Katu sikuwahi kuona kabla maji ya mto rangi hii.

**Soloman:** Hebu niambie lini ilinyesha mvua kubwa mara ya mwisho ?

**Moses:** Jana usiku. Kulikuwa na ngurumo za mvua, ziliniamsha.

**Soloman:** Hasa! Mvua ilinyesha kwa nguvu sana ikasomba sehemu ya juu ya ardhi yenye virutubishi hadi chini mlimani na hatimaye kufikia mtoni. Hivi sasa mto huo umejaa masimbi na unabadili rangi ya maji

**Gladys:** Familia yangu ilikuwa imezoea kulima karibu na hapa na kulikuwa na ziwa hapo sehemu ya chini tu ya mto.

**Soloman:** Sawa kabisa.

**Gladys:** Na lilikuwa na maji safi yanayong’ara.

**Soloman:** (Hum of agreement … sauti ya kukubali ) Hmmmmm nakumbuka.

**Gladys:** Hivi sasa ni tafauti kabisa. Linaonekana kujaa matope.

**Soloman:** (sigh kwa majonzi) Unajua ziwa hilo kina chake kwenda chini kilikuwa mita 10. Hivi sasa kina chake ni mita mbili tu.

**Monica:** Kwa sababu limejaa mchangatope?

**Soloman:** Nahofia hivyo

**Gladys:** Je hali hiyo inawaathiri jamii ya wavuvi katika ziwa?

**Soloman:** Bila ya shaka inawaathiri. Ziwa hilo linanyauka na idadi ya samaki inapungua.

**Moses:** Kutokana na ukweli kwamba mbao yetu ni rasilimali ya thamani ambayo mataifa yalioendelea yanataka kuitia mikononi inawezekana kukata miti katika njia ambayo haiharibu mazingira?

**Soloman:** Ndiyo kuna hoja kwamba ukataji wa miti unaweza kuwa endelevu iwapo utakata baadhi ya miti na sio yote katika njia mbayo haitosababisha madhara makubwa kwao. Hii inawezesha miti mingine kukua kwa nguvu zaidi na kuhakikisha kwamba mizizi ya miti inashikilia ardhi pamoja.

**Moses:** Na inamaanisha kwamba unatunza makaazi ya wanyama!

**Moses:** Ukataji miti endelevu inaonekana kama ni kupiga hatua mbele.

**Music — 0:30**

**Je ulikuwa ukijua?**

Kila mwaka Afrika inapoteza asilimia 0.7 ya jumla ya misitu yake. Baadhi ya wanasayansi wanasema takwimu inaweza kuwa kubwa kuliko hata hiyo. Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa,m Afrika imepoteza asilimia kubwa kabisa ya misitu ya joto kuliko bara lolote lile duniani katika miaka ya 1980, 1990 na mapema miaka ya 2000. Kwa jumla kama hekta milioni 23 za misitu zimetoweka katika miaka ya 1980 na hekta milioni 20 imepotezwa katika miaka ya 1990. Sehemu kubwa ya misitu ya majira ya joto barani Afrika inapatikana Afrika Magharibi na Afrika ya Kati.

Wakati misitu inapokatwa, kima cha maji kinachotembea juu ya ardhi kinaongezeka sana kwa sababu kima kikubwa cha maji ya mvua kinafika kwenye ardhi. Utafiti umebaini kwamba misitu ya joto inaweza kupata maji mengi kwa saa sawa na yale inayotegemea kupata London katika kipindi cha mwezi mmoja wa mvua. Utafiti huo pia umeonyesha kwamba mvua moja kubwa imepimwa kusomba tani 185 za sehemu ya juu ya ardhi kwa kila hekta. Hali hiyo huitwa mmomonyoko wa udongo. Mmommonyoko wa udongo unaelezewa kuwa ni kuondolewa au kusombwa kwa masimbi, jabahi na mchanga kutoka kwenye ardhi.

Ni muhimu kukumbuka kwamba mmommonyoko wa udongo moja kwa moja ni mchakato wa asili. Hata hivyo utaratibu huo unaweza kuharakishwa kwa njia isio ya asili yaani harakati za binaadamu. Ukataji wa miti ni mojawapo ya harakati hizo ambazo huathiri moja kwa moja viwango vya mmommonyoko wa udongo kusini mwa jangwa la Sahara barani Afrika.Maji ni kile wanasayansi wanachoklita kuwa mhusika mkuu kabisa wa mmommonyoko wa udongo. Kwa maeneo mengine maji mara nyingi yale ya mto husafirisha masimbi mengi kutoka kwenye ardhi na kupeleka baharini kila mwaka kuliko hata barafu au upepo ambavyo ni vitu vingine viwili vya asili vinavyohusika na mmommonyoko wa udongo. Lakini wakati mmommonyoko wa udongo wa asili ni mchakato wa taratibu wa hatua kwa hatua kama tulivyosikia unaweza kuharakishwa na harakati za binaadamu kama vile ukataji wa miti.

Baadhi ya nyakati katika hali zinaonekana kuwa mbaya kabisa matokeo yake ni kwamba kima kikubwa cha vitu huondolewa au kusombwa na sura ya ardhi kwa ghafla huundwa upya. Matukio ya hali hizo ni pamoja na maporomoko ya ardhi ambayo hutokea mara kwa mara katika nchi ambazo mvua za joto kwa haraka zinaweza kurowesha milima na kutokana na miaka mingi ya ukataji wa misitu inamaanisha kwamba kuna mimea michache inayoweza kuutuliza na kuufanya udongo ushikamane.Bila ya kuwepo kwa safu ya virutubishi ya juu ya udongo ardhi inayokuweko chini inakuwa haina rutuba. Jambo hili linamaanisha kwamba katika kipindi cha usoni itachukuwa karne nyingi kwa misitu kurudi katika hali yake ya kawaida na kuiacha taswira ya ardhi ya kutisha isiofutika kwa kizazi kijacho.

**Outro ...Funga kipindi**

Na hapo ndio tumefikla mwisho wa vipimdi vyetu maalum. Sikiliza na Ujifunze kuhusu mazingira ambapo leo tumelenga ukataji wa misitu. Asante kwa kuwa nasi na kumbuka kwamba unaweza ukayapata yote yaliomo kwenye kipindi hiki kwenye mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe.
Kwa heri.